

Mfululizo wa Masuala ya Kifikihi

al-Qasir fi - 's-Safar

'Alaa Dhaw'i 'l-Kitaab wa 's-Sunnah

Kupunguza Swala Safarini

KWA MUJIBU WA KITABU NA SUNNA

Kimeandikwa na:

Sheikh Ja'far Subhani

Kimetarjumiwa na:

Hemedi Lubumba Selemani

© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 427 - 59 - 8

Kimeandikwa na:
Sheikh Ja'far Subhani

Kimetarjumiwa na:
Hemedi Lubumba Selemani

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Kupangwa katika Kompyuta na:
Ukhti Pili Rajab.

Toleo la kwanza: Machi, 2008
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info

YALIYOMO

Je kupunguza safarini ni lazima au ni hiyari.....2

Dalili za wanaosema kuwa kupunguza ni wajibu kwa mujibu wa Sunna.....10

Kupunguza swala Mina.....20

Dalili za wanaodai kuwa kupunguza ni ruhusa ya Hiyari..... 25

Kutoa hoja kwa kutumia kitendo cha Uthman na Aisha.....34

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "*Al-Qasir fi 's-Safar*" Sisi tumekiita: "**Kupunguza Swala Safarini.**"

Kitabu hiki, "**Kupunguza Swala Safarini**" ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanywa na Mwanachuoni wa Kiislamu, **Sheikh Jafar Subhany.**

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake.

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilinganisha na yale tunayokubaliana nayo.

Kupunguza Swala Safarini: Hili ni suala ambalo wanachuo wetu wamehitalifiana; ndani ya madhehebu moja na kati ya madhehebu. Kwa hiyo hii sio hitilafu ya madhehebu, bali ni hitilafi ya wanachuo wa madhehebu zote, wamehitilafiana juu ya suala hili. Lakini bahati mbaya Waislamu wengi hawaitambui hitilafu hii kwa usahihi na hivyo kuogelea katika dhana na kusababisha mizozo isiyokuwa na maana. Kutokana na hali hii Sheikh wetu, Jafar Subhani amelifanyia

utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi asili ya hitilafu hii, kisha akamuachia msomaji mwenyewe kutoa uamuzi.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Hemedi Lubumba Selemani** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 19701

Dar-es-Salaam, Tanzania.

KUPUNGUZA SAFARINI KWA MUJIBU WA KITABU NA SUNNA

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mlezi wa ulimwengu. Rehma na Amani zimfikie mbora wa viumbe na hitimisho la mitume wake, pia kizazi chake kitakatifu ambacho ndio kasha la elimu yake na hazina ya mafunzo yake.

Hakika Uislamu ni imani na sheria. Imani ni kuamini Mwenyezi Mungu, mitume wake na siku ya mwisho. Na sheria ni hukumu za Mwenyezi Mungu ambazo zina jukumu la kumpa mwanadamu maisha bora na kumuhakikishia wema wa dunia na akhera.

Sheria ya kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ

الْإِسْلَامَ دِينًا ﴿٥﴾

“Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu.” (5:3).

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanachuoni wa sheria wametofautiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo

ambalo limepelekea kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya tumejaribu kuliweka swala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu, kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata ipelekee kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za kiisilamu.

Na muongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

﴿وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۗ وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ


أَعْدَاءَ فَأَلْفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِ ۗ ﴿١٣﴾

“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema zake mkawa ndugu.”
(3:103).

Jafar Subhany

Taasisi ya Imam Sadiq (a.s.)

Qum



JE KUPUNGUZA SAFARINI NI LAZIMA AU NI HIYARI

Kwa mujibu wa Kitabu na Sunna waislamu wameafikiana juu ya sheria ya kupunguza safarini hata kama mpunguzaji hana khofu. Isipokuwa tofauti ni kuwa je kupunguza safarini ni wajibu au Sunna iliyohimizwa? Au je ni ruhusa ya hiyari?

Hapa kuna kauli tatu tutakazoashiria kwa ufafanuzi: Imamiya na Hanafiya wamesema kuwa ni wajibu, na kuwa faradhi ya msafiri katika kila Swala ya rakaa nne ni kuswali rakaa mbili.

Malikiya wakesema: “Kupunguza ni Sunna iliyohimizwa kutokana na kitendo cha Mtume kwani hajawahi kuonekana akitimiza Swala safarini.

Mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) wamepokea toka kwa Ibnu Umar kuwa alisema: “Niliishi na Mtume na alikuwa hazidishi rakaa mbili safarini, na Abubakri na Umar nao walikuwa hivyo hivyo.”¹

Shafiiya na Hambaliya wamesema: “Kupunguza ni ruhusa ya hiyari, hivyo msafiri ana hiyari akitaka apunguze au atimize.”

Sheikh Tusi ndani ya *Al-Khilafu* amesema: “Kupunguza safarini ni faradhi na wajibu, hivyo wajibu katika Swala hizi tatu: Adhuhuri, alasiri na isha ni rakaa mbili, hivyo iwapo ataswali rakaa nne ilihali anajua basi itamlazimu kurudia Swala.”

1-*Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi Jz: 5, uk. 205. Kitabu cha Swala namba 5.Mlango wa Swala ya msafiri na kupunguza kwake.

Kupunguza Swala Safarini

Abu Hanifa naye akasema kama tulivyosema isipokuwa yeye kaongeza: Iwapo atazidisha rakaa mbili basi iwapo alitoa tashahudi katika rakaa ya pili Swala yake ni sahihi, na rakaa mbili zilizozidi zitakua ni Swala ya Sunna. Isipokuwa atakaposalishwa na imamu asiye safarini kisha akaswali rakaa nne hapo rakaa zote nne kwa pamoja (mbili za mwanzo na mbili za pili) zitakuwa ni faradhi husika, hivyo zitakuwa zimetosheleza faradhi husika.

Na kauli ya kuwa kupunguza ni wajibu ndio madhehebu ya Ali na Umar. Na katika wanachuoni wa sheria ni madhehebu ya Abu Hanifa na jamaa zake.

Shafiy amesema: “Ana hiyari kati ya kuswali Swala ya safari rakaa mbili au asali Swala isiyo ya safari rakaa nne, kwa kufanya hivyo anakuwa kaondokewa na faradhi.”

Shafiy amesema: “Kupunguza ni bora.”

Al-Mazniy amesema: “Kutimiza ni bora, kauli hii ndio kauli ya maswahaba: Uthmani, Abdallah bin Mas’udi, Sa’d bin Abi Waqasi, na Aisha. Ama katika wanachuoni wa sheria imesemwa na Al-Awzaiiy na Abu Thauru. ²

Hizi ndio kauli

Kisha uchambuzi kuhusu Swala ya msafiri ni suala pana, kwani kuna uchambuzi kuhusu masafa ambayo inasihhi kupunguza ndani yake, na kuna uchambuzi kuhusu namna ya safari inayosihhi kupunguza, na pia je kupunguza ni mahususi kwa safari ya utiifu au inajumuisha safari ya maasi?

2- *Al-Khilafu*: 1/ 569. Kitabu cha Swala. Suala la 321

Kupunguza Swala Safarini

Tatu: Uchambuzi kuhusu eneo analoanzia msafiri kupunguza.

Nne: Ni uchambuzi kuhusu kiwango cha muda ambao iwapo msafiri atakaa sehemu kwa kiwango cha muda huo basi atatimiza Swala.

Kwani wapo wanaosema kuwa akinuwia kukaa mahali siku nne basi inatosha kutimiza, hiyo ni kauli ya Malikya na Shafiya. ³

Na wapo wanaosema kuwa atapunguza isipokuwa atakaponuwia kukaa sehemu muda wa siku kumi, hiyo ni kauli ya Imamiya.

Na kuna uchambuzi mwingine mwingi unaohusu Swala ya msafiri. Lakini sisi hapa tutakazania mada nyingine ambayo ni je kupunguza ni wajibu au Sunna iliyohimizwa au je ni ruhusa ya hiyari?

Hatutoingia katika hizo mada nne wala hatutoingia katika sharti za kupunguza zilizotajwa na wanachuoni wa sheria, kwa sababu uchambuzi juu ya mada hizo unatupelekea kuandika kitabu maalumu na tayari tumeshaziandika mada hizo katika kitabu kilichochapishwa kuitwacho ‘*Dhiyaul-Nadhiru fi swalati musafiri*’ yaani, Mwanga wa mtafiti kuhusu Swala ya msafiri.

Baada ya kujua hayo hebu sasa tuingie ndani ya mada husika.

Ama ndani ya kitabu ni kuwa Mwenyezi Mungu amesema: **“Na mnaposafiri katika ardhi, basi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala, iwapo mkiogopa ya kwamba wale waliokufuru wataku-peni taabu. Hakika makafiri ni maadui wenu walio wazi.”** ⁴

3- *Al-Fiq'hi Al-Islamiy: 2/ 338-339*. Imenukuliwa toka As-Shar'hu Al-Kabir wa mugh'nil-muhtaji.

4- **An-Nisaa:101**

Kupunguza Swala Safarini

Misamiati ya Aya

Adharbu fil-ardhi: Ni kinaya cha safari, maana yake mtakapokuwa safarini si vibaya kwenu - yaani si makosa – wala si dhambi kupunguza Swala – yaani: idadi yake - hivyo Swala za rakaa nne mziswali rakaa mbili mbili.¹ (1)

Pia hii ndio tafsiri aliyofasiri Qurtubiy ndani ya kitabu *Al-jamiu liahkamil-Qur'an*² kinachounga mkono tafsiri hiyo ni kutumika msamiati: *Dharbi fil-ardhi* katika Aya zaidi ya moja mfano Aya: “Enyi mlioamini, mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu basi pelelezeni.”³

Akasema katika Aya nyingine: “Mnapokuwa safarini na msiba wa mauti ukakifikieni.”⁴

Akasema tena: “Waliposafiri katika nchi au walipokuwa vitani, wangukuwa kwetu wasingekufa wala wasingeliwa.”⁵

Ama *Al-junahu*: Maana yake ni kosa hiyo ni kama ilivyo katika ibara ya Shekhe ndani ya *At-Tibyani*, na neno hilo limetumika sana ndani ya Aya nyingi kwa maana ya kosa. Mwenyezi Mungu amesema: **“Basi mwenye kuikusudia Al-Kaaba au kuizuru si vibaya kuizunguka.”**⁶

1. *At-Tibyani fi tafsiril-Qur'an*:3/307

2. *Al-Jamiu liahkamil-Qur'an*: 5/ 351

3. **An-Nisaa: 94**

4. **Al-Maida:106**

5. **Al-Imran:156**

6. **Al-Baqara:158**

Kupunguza Swala Safarini

Neno *Junahu* ndani ya Qur'an limetumika mara ishirini na tano na katika mara zote hizo linakusudiwa kosa.

Hakika sentensi: 'Si vibaya kwenu' ni matokeo ya sharti lililotangulia. Hivyo ni kama kasema: Iwapo mkiogopa kuwa waliokufuru watakupeni taabu basi si vibaya kwenu kupunguza Swala.

Makusudio ya kupunguza ni kupunguza idadi ya raka za toka raka nne hadi raka mbili. Huenda mtu akafasiri kupunguza kwa maana ya kupunguza namna na sifa ya Swala kwa kubadili ruku na sujudu iwe kwa kuashiria.

Au kuswali ilihali uko juu ya kipando au ukitembea kulingana na hali husika iliyokufika kama vile ilivyo katika Swala ya khofu na kufukuzwa.

Baadhi ya wapokezi wamenasibisha maana hiyo kwa Ibnu Abbas na Ibnu Jariru toka kwa Ibnu Tausi toka kwa baba yake. Na ndio aliyogemea Abu Bakr Al-Jasasu katika tafsiri yake.⁷

Na huenda ndio inayodhihiri toka kwa As-Sayyid Al-Murtadha ndani ya '*Intiswari*'⁸ na kwa Al-Qutubi Al-Rawandiy ndani ya '*Fiqihul-Qur'an*'⁹

Lakini lililo maarufu kwa wafasiri wa Qur'ani na ndilo lililomo ndani ya riwaya za Ahlul-Baiti ni kuwa makusudio ya kupunguza ni kupunguza idadi ya raka za Swala za raka nne, hivyo tamko '*Min*' katika kauli: '*Mina swalati*' limetumika kwa maana ya baadhi yaani sehemu, hivyo maana yake ni sehemu ya Swala.

7. *Ahkamul-Qur'an*: 2/259

8. *Al-Intiswari*:53

9. *Fiq'hul-Qur'an*:516

Kupunguza Swala Safarini

Ama kufanya tamko ‘*Min*’ kuwa ni tamko la ziada kama alivyonukuu Abul-Maqaq toka kwa Al-Akhfashi kuwa ni tamko la nyongeza baada ya kuthibitisha jukumu, hakika matumizi hayo hayakubaliani na Kitabu kitukufu.¹⁰

Kisha Aya inahusu kupunguza kwenye safari yenye khofu, hivyo dhahiri ni kuwa safari pekee sio sababu tosha ya kupunguza bali sababu tosha ni safari yenye khofu. Lakini Sunna imetafsiri na kuifanya safari pekee kuwa sababu tosha ya kupunguza.

Hakika Mtume alikuwa akipunguza katika hali zote mbili, ya khofu na ya amani kama tutakavyoona katika riwaya. Ama kiten-do cha kupunguza kuegemezwa na khofu katika aya hiyo, ilikuwa ni kutaka kuripoti hali halisi kwani mara nyingi safari za Mtume zilikuwa hazikosi khofu.

Kwa ibara nyingine ni kuwa sharti lililopo katika aya hiyo ni sharti la hali ya mara kwa mara linalohusu mazingira iliyoshukia aya, hivyo atakayetaka kuhusisha kitendo cha kupunguza na safari yenye khofu tu na kuivua safari yenye amani atakuwa amechukua dhahiri huku akiwa ameiacha Sunna ya Mtume na makubaliano ya waislamu ambao wa kwanza wao ni Maimamu wa kizazi cha Mtume ambao Mtume aliwatambulisha kwetu akasema wao ni pacha wa Qur’ani na waambata wa Kitabu.

Kisha atakayedai kuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari atakuwa kashikilia dhahiri ya aya nayo ni kauli: ‘Si vibaya kwenu’ laki-ni ameghafilika kuwa tamko hili halionyeshi makusudio yake, kwa sababu Aya imekuja kuondoa dhana ya uharamu, hivyo ni kama muambiwaji anadhania kuwa kupunguza Swala ni jambo la haramu, hivyo ikateremka Aya kuondoa dhana hii ili atulie na

10. Amenukuu toka kwa Abul-Baqai Al-Aluwsiy ndani ya *Ruhul-Maaniy*: 5/131

Kupunguza Swala Safarini

kutuliza moyo wake apunguzapo.¹¹

Hilo si geni kwani jambo kama hilo limepatikana pia katika kauli ya Mwenyezi Mungu: **“Hakika Swafa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu, basi mwenye kuikusudia Al-Kaaba au kuizuru, si vibaya kuizunguka. Na mwenye kufanya kheri basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushukuru, Mjuzi.”**¹²

Hakika walipotaka waislamu kutufu kati ya Swafa na Marwa katika Umra ya kulipa waliona kuna masanamu juu ya Swafa na Marwa hivyo waislamu wakaona ni dhambi kuitufu, hapo ikateremka kauli ya Mwenyezi Mungu: “Hakika Swafa na Marwa ni alama za Mwenyezi Mungu.”

Tabarasiy anasema: “Juu ya Swafa kulikuwa na sanamu liitwalo Isafu, na juu ya Marwa kulikuwa na sanamu liitwalo Naila, na mushirikina wanapokuwa juu ya milima hiyo walikuwa wakiyagusa, hivyo waislamu wakaona ni dhambi kuitufu milima hiyo kwa ajili ya masanamu hayo mawili. Ndipo ikateremka Aya hii.”

Haya ndiyo yalinyonukuliwa toka kwa As-Shaabiy na toka kwa wanachuoni wengi, hivyo kitendo cha kuondoa ubaya wakati wa kutufu kinahusu ile dhana ya dhambi iliyotokana na kuwepo masanamu wakati wa kutufu, wala hakihusu kutufu kwenyewe.

Hali hiyo ni sawa na mtu aliyefungwa sehemu ambayo hawezi kuswali ispokuwa kwa kuelekea sehemu isiyoruhusiwa kuelekea. Hivyo huambiwa: Si vibaya kwako kuswali ilihali umeelekea sehemu hiyo, hivyo kitendo cha kuondoa ubaya hakihusu Swala

11. *Al-Kashafu*:1/294 chapa ya Darul-maarifa

12. **Al-Baqara: 158**

Kupunguza Swala Safarini

enyewe kwa sababu Swala yenyewe ni wajibu bali kinahusu kuelekea sehemu hiyo.

Riwaya nyingine imepokewa toka ka Aba Abdillah (a.s.) kuwa hilo lilitokea kwenye Umra ya kulipa baada ya Mtume kuwapa sharti kuwa kabla ya kutufu kwanza waondoe masanamu, hapo mmoja wa maswahaba zake akajishughulisha na jambo lingine mpaka masanamu yakarudishwa.

Wakaja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumwambia kuwa fulani hajatufu ilhali masanamu yamesharudishwa, ndipo ikateremka aya hii (Si vibaya kuizunguka) maana yake, huku masanamu yakiwa juu yake. Akasema: “Hivyo watu wakawa wakiizunguka ilhali masanamu yakiwa kama yalivyo.”¹³

Hali hiyo hiyo ndio hali ya mada yetu, kwani hakika kupunguza Swala na kuibadili kuwa rakaa mbili ni kati ya mambo ambayo muislamu anadhani ni dhambi na kuwa ameacha faradhi husika, hivyo katika hali kama hii Mwenyezi Mungu anasema: **“Na mnaposafiri katika ardhi, basi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala.”**

Hivyo kutokana na maelezo hayo ni kuwa Aya haijulishi wajibu wala ruhusa ya hiyari bali yenyewe haijazungumzia chochote kuhusu mawili hayo.

Mpaka hapa imebainika kuwa Aya haijulishi kauli yoyote kati ya hizo, hivyo hatuna kimbilio isipokuwa ni kurejea kwenye Sunna tukufu.

13. *Majmaul-bayani*:1/240 katika tafsiri ya Aya hiyo

Kupunguza Swala Safarini

DALILI ZA WANAOSEMA KUWA: KUPUNGUZA NI WAJIBU KWA MUJIBU WA SUNNA

Sunna nyingi zilizoenea ndani ya *Sahihi sita*, vitabu vya Sunna na vitabu vya Hadith zinaonyesha kuwa kupunguza ni lazima na kuwa Mtume alikuwa akipunguza katika safari zake zote. Hapa tunataja chache kati ya hizo nyingi.

Muslim amepokea toka kwa Aisha mke wa Mtume kuwa alisema: “Swala ilifaradhiwa rakaa mbili mbili safarini na pasipo safarini, hivyo ikasitishwa Swala ya safari na kuzidishwa Swala isiyo ya safari.”¹⁴

As-Shaukaniy amesema: “Nayo ni dalili iliyosimama juu ya wajibu, kwa sababu iwapo Swala ya msafiri imefaradhiwa kwa rakaa mbili haisihi kuzidisha zaidi ya hapo kama vile isivyosihhi kuzidisha zaidi ya rakaa nne kwenye Swala ya asiye safarini.”

Kisha yule aliyetaka kuilazimisha riwaya inyenyekee kwa mujibu wa fiqih ya madhehebu yake amehoji riwaya hiyo kwa hoja mbovu ambazo zimenukuliwa na As-Shaukaniy ndani ya kitabu chake. Na yafuatayo ni maelezo yake:

Hakika kauli kutoka kwa Aisha imevushwa (yaani haionyeshi Aisha kaitoa kwa nani) na yeye hakushuhudia pindi ambapo Swala ilifaradhiwa. Laiti Hadithi hii ingethibiti basi ingenukuliwa kwa wingi (*Tawaturi*).

Anajibiwa kuwa: Kipimo ni uadilifu wa mpokezi sawa awe amesikia moja kwa moja toka kwa Mtume au amesikia toka kwa muadilifu

14. *Shar'hu Sahihi Muslim* ya An-Nawawi:5/201. *Sahihi Bukhari*:2/55 kitabu cha Swala, mlango wa kupunguza atakapo kwake.

Kupunguza Swala Safarini

mwingine.

Na laiti katika kuchukua riwaya za Aisha tukisema tukomee katika zile za kipindi alichokuwa na Mtume basi sehemu kubwa ya riwaya zake zitakuwa hazifai, kwani mara nyingi amekuwa akipokea matukio ambayo hakuyashuhudia, Na hapa tutatoa riwaya moja tu kama mfano, nayo ni riwaya inayohusu namna ulivyoteremka wahyi kwa Mtume.

Bukhari ameinikuu ndani ya *Sahih* yake kwa ufafanuzi: Mtume alikuwa akienda pango la Hira mwezi mmoja kila mwaka mpaka ulipofika mwezi ambao Mwenyezi Mungu alimkabidhi utume, hivyo Mtume wa Mwenyezi Mungu akatoka mpaka pango la Hira akabaki huko mpaka ulipofika usiku ambao Mwenyezi Mungu alimkirimu kwa utume, akaja Jibril na amri ya Mwenyezi Mungu.

Hebu tuache maelezo hayo na twende kwenye yale aliyopokea kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu, akasema: Akanijia Jibril ilihali nikiwa nimelala akiwa na kitabu akasema: “Soma.” Nikasema: Nisome nini? Hapo akanibana mpaka nikadhani kifo kimenifika kisha akaniachia.

Akaniambia: “Soma.”

Akasema: Nikasema: Nisome nini? Hapo akanibana mpaka nikadhani kifo kimenifika kisha akaniachia.

Akaniambia: “Soma.”

Akasema: Nikasema: Nisome nini ?..... ¹⁵

Angalia jinsi anavyovusha (haonyeshi yeye kaitoa kwa nani) riwaya ya jinsi wahyi ulivyoteremka kwa Mtume japokuwa kipindi hicho alikuwa hajazaliwa.

15. *Sahih Bukhari*:1/3 na 3/173 katika tafsiri ya **Surati Al-Alaq**

Kupunguza Swala Safarini

- b) Makusudio ya kauli ya Aisha: Ilifaradhiwa: Maana yake ilikadiriwa.
- c) Makusudio ya kauli ya Aisha: Ilifaradhiwa, maana yake kwa yule anayetaka kupunguza, hivyo zikazidishwa kwa namna ya wajibu rakaa mbili katika Swala asiyo ya safari na ikasitishwa Swala ya safari kwa kusihhi kupunguza. ¹⁶

Anajibiwa kuwa: Hakika hoja zote mbili ni kuiondoa dalili kwenye msitari wake nayo ni tafsiri ya rai binafsi jambo ambalo halikubaliki katika kutafsiri maneno ya Mwenyezi Mungu au maneno ya Mtume Wake au maneno ya mtu mwingine.

Muslim amepokea toka kwa Aisha kuwa Swala ilipofaradhiwa mwanzo ilikuwa ni rakaa mbili, hivyo ikasitishwa Swala ya safari na ikatimizwa Swala isiyo ya safari. Az-Zahriy amesema: Nikamwambia Urwa : Vipi Aisha, mbona yeye anatimiza safarini? Akasema: Hakika yeye alibeua tafsiri kama alivyobeua Uthman. ¹⁷

Yatakufikia maneno kuhusu Aisha kutimiza safarini.

Muslim amepokea toka kwa Ibnu Abbas kuwa alisema: “Mwenyezi Mungu alifaradhiwa Swala kwa ulimi wa Mtume wenu, pasipo safarini rakaa nne na safarini rakaa mbili na katika hali ya khofu rakaa moja.”

Muslim amepokea toka kwa Musa bin Salama Al-Hadhaliy kuwa alisema: “Nilimuuliza Ibnu Abbas: Niswali vipi nitakapokuwa Makka iwapo siswali na imamu? Akajibu: “Rakaa mbili Sunna ya Abul-

16. *Naylul-awtari*: 3/201

17. *Shar'hu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/201.

Kupunguza Swala Safarini

Qasimu (Mtume s.a.w.w.)”

Muslim amepokea toka kwa Isa bin Hafsa bin Aswimu bin Umar bin Al-Khattab toka kwa baba yake kuwa alisema: Nilikuwa na Ibnu Umar safari ya kuelekea Makka. Akasema: Akatuswalisha Adhuhuri raka mbili. Akaendelea mpaka akasema: Mimi nilisafiri na Mtume wa Mwenyezi Mungu wala hakuwali zaidi ya raka mbili mpaka alipofariki. Na nikasafiri na Abu Bakr wala hakuwali zaidi ya raka mbili mpaka alipofariki. Na nikasafiri na Umar wala hakuwali zaidi ya raka mbili mpaka alipofariki. Na nikasafiri na Uthman wala hakuwali zaidi ya raka mbili mpaka alipofariki. Kwani Mwenyezi Mungu amesema: “Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Muslim amepokea toka kwa Anas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali Adhuhuri Madina raka nne na akasali Alasiri Dhawil-halifa raka mbili.

Muslim amepokea toka kwa Yahya bin Yazid Al-Hanaiy amesema: Nilimuuliza Anas bin Malik kuhusu kupunguza Swala. Akasema: “Mtume alikuwa atokapo safari ya maili tatu au farsakhu tatu (Tawi la mwenye shaka) huswali raka mbili.

Dhahiri ya Hadithi ni kuwa mwanzo wa kupunguza ni baada ya kutembea maili tatu. Na lililo mashuhuri ni kinyume na hivyo.

An-Nawawi amesema: “Hili sio sharti isipokuwa lilitokea kulingana na mahitaji, kwa sababu linalodhihirika katika safari zake ni kuwa alikuwa hawi na safari ndefu kisha aanze safari pindi inapofika faradhi inayostahili kupunguzwa eti ili asipunguze bali atimize kwa kuwa yuko karibu na Madina.

Kupunguza Swala Safarini

Bali alikuwa akisafiri mbali na wakati wa faradhi inayostahili kupunguzwa hivyo faradhi inamkuta akiwa ametimiza maili tatu au zaidi, hivyo anawajibika kuswali muda huo.

Hadithi na dhahiri ya Qur'an zinaungana mkono juu ya ruhusa ya kupunguza pindi anapotoka mjini, hivyo wakati huo huitwa msafiri.¹⁸

Muslim amepokea toka kwa Jubairi bin Nafiru alisema: “Nilitoka na Sharhabilu bin As-Simtu kwenda kijiji cha umbali wa maili kumi na saba au kumi na nane akaswali raka mbili. Nikamuuliza kuhusu hilo, akanijibu: “Nilimuona Umar akiswali raka mbili Dhul-Halifa nami nikamuuliza akasema: Hakika ninafanya kama nilivyomuona Mtume akifanya.”

Hadith hii inaonyesha kuwa daima Mtume alikuwa akipunguza safarini, isipokuwa tofauti ni kuwa je mwanzo wa kupunguza ni kutoka tu mjini kama ilivyokuwa kwa Umar, au mwanzo ni baada ya kutoka mwendo wa maili kumi na nane.

An-Nawawi amesema: Ama kauli ya kuwa: “Alipunguza Sharhabilu bin As-Simtu akiwa umbali wa maili kumi na saba au kumi na nane” si hoja kwa sababu yeye alikuja baada ya maswahaba na amefanya jambo lililo kinyume na jamhuri yote. Au alifasiri kuwa kupunguza kulikuwa ndani ya safari na wala si mwisho wa safari yake, na tafsiri hii ni ya juu juu.¹⁹

Vyoyote vile ni kuwa sehemu hii ya tofauti iko nje ya uchambuzi wetu.

18. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/207

19. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/207

Kupunguza Swala Safarini

Muslim amepokea toka kwa Anas bin Malik amesema: Tulisafiri na Mtume wa Mwenyezi Mungu toka Madina kuelekea Makka akaswali rakaa mbili mbili mpaka tuliporejea, nikamwambia: Alikaa siku ngapi Makka? Akasema: “Kumi.”

Kisha kitendo cha Mtume kupunguza Makka ilihali akikaa siku kumi Makka japokuwa kinaafikiana na baadhi ya madhehebu lakini kinapingana na madhehebu ya Imamu Malik kama kinavyopingana na madhehebu ya Shia Imamiya, kwani hakika nia ya siku kumi inavunja safari na inawajibisha kutimiza. Na huenda haikuwa kumi kamili iliyotimia bali kumi ya kijamii ambayo ilipungua kidogo katika kumi kamili.

Hizi ni Hadith tisa alizonukuu Muslim ndani ya *Sahih* yake, na zifuatazo ni walizonukuu wengine:

Abu Malik amepokea toka kwa Imrani bin Al-Huswaini, alisema: Nilipigana pamoja na Mtume nikashuhudia ukombozi wa Makka nikiwa nae, akakaa Makka siku kumi na nane ilihali haswali isipokuwa rakaa mbili huku akisema: “Enyi wakazi wa mji huu, swalini rakaa nne hakika sisi ni wasafiri.”²⁰

Katika Hadith hii tunachukua kipengele cha mwanzo. Ama kilichonasibishwa na Mtume kuwa alikaa siku kumi na nane hasali isipokuwa rakaa mbili chenyewe kinapingana na alichonukuu Anas kuwa alikaa Makka siku kumi.

20. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/8 *Sunnani Abu Daudu*:2/10 namba 1229 na *Sunnanil-Tirmidhiy*:2/430 namba 545

Kupunguza Swala Safarini

Vyovyote vile itakavyokuwa ni kuwa mkazo wa Mtume juu ya kupunguza akiwa Makka muda wote aliyokaa humo (huku akiwa katika lengo la kuwafundisha hukumu za Swala watu wa Makka ambao walikuwa wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi) ni dalili ya kuwa kupunguza ni lazima na kama si hivyo basi angetimiza Swala kwa sababu kufanya hivyo ndio kungekuwa kunalingana na hali ya kutoa mafunzo, hiyo ni kwa ajili ya upekee wa imamu huku Swala ya maamuma ikimfuata yeye pekee katika idadi na namna.

Ibnu Maja amepokea ndani ya *Sunnan* yake toka kwa Umar kuwa alisema: Swala ya safari na Swala ya Ijumaa ni rakaa mbili, Swala ya Idi ndogo na Idi kubwa ni rakaa mbili kamili si pungufu, kwa kauli ya Muhammadi (s.a.w.w.).²¹

At-Tabaraniy ametoa toka kwa Ibnu Abbas ambaye alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alifaradhisha rakaa mbili safarini kama alivyofaradhisha rakaa nne pasipo safarini.”²²

Kuna riwaya nyingine zimeenea ndani ya vitabu vya fiq’hi, na yafuatayo ni maelezo yake:

Imepokewa toka kwa Swafwani bin Mihrazi kuwa alimuuliza Ibnu Umar kuhusu Swala safarini. Akasema: “Ni rakaa mbili, atakayeenda kinyume na Sunna kakufuru.”²³

Imepokewa toka kwa Ibnu Umar kuwa alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alituijia ilihali sisi tukiwa tumepotea sana hivyo akatufunza, na miongoni mwa aliyotufunza ni kuwa Mwenyezi

21. *Al-Sunmani*:1/338 namba 1036

22. *Nasbul-rayati*:2/189

23. *Al-Mughuniyu*:2/107

Kupunguza Swala Safarini

Mungu ametuamrisha tusali raka'a mbili safarini.”²⁴

Umar bin Abdul-Aziz amesema: “Swala ya safarini ni raka'a mbili tu, haifai nyingine.”²⁵

Toka kwa Umar bin Al-Khattab toka kwa Mtume alisema: “Swala ya msafiri ni raka'a mbili mpaka arudi kwake au afariki.”²⁶

Toka kwa Ibrahim amesema kuwa Umar bin Al-Khattab aliswali adhuhuri raka'a mbili Makka alipomaliza akasema: ‘Enyi watu wa Makka hakika sisi ni wasafiri, hivyo mkazi wa mji huu atimize, hapo wakatimiza wakazi wa mji.’²⁷

Toka kwa Abil-Kunudi Abdallah Al-Azdiy amesema: Nilimuuliza Ibnu Umar kuhusu Swala ya safarini. Akasema: ‘Ni raka'a mbili zilizoteremka toka mbinguni, mkitaka zikataeni.’²⁸ Hadithi hii inafichua kuwepo kwa mvutano kati ya nyayo na ugoko yaani kati ya maswahaba na waliyokuja baada ya maswahaba.

Toka kwa Al-Swaibu bin Yazidi Al-Kindiy amesema: “Swala ilifarad-hishwa raka'a mbili mbili kisha zikazidishwa katika Swala isiyo ya safari na zikasitishwa katika Swala ya safari.”²⁹

Imepokewa toka kwa Ibnu Mas'udi kuwa amesema: “Atakayeswali safarini raka'a nne atatakiwa kurudia Swala.”³⁰

24. *Naylul-awtari*:3/204 Amesema: Ameipokea An-Nasaiy

25. *Al-Mughuniyu*:2/108. *Al-Mahaliyu*: 4/271

26 *Ahkamul-Qur'an ya Al-Jasasu*: 2/254

27. *Al-Athari*: 30 na 75 ya Abu Yusufu kama ilivyo ndani ya *Al-Ghadir*:8/113

28. *Maj-maul-Zawaid*: 2/154. Amesema: Na wapokezi wake ni waaminifu

29. *Majmauz-Zawaid*: 2/155. Na imeshatangulia Hadith kama hii toka kwa Aisha *Majmauz-Zawaid*: 2/155

30. *Majmauz-Zawaid*: 2/155.

Kupunguza Swala Safarini

Toka kwa Salmani amesema: “Swala ilifaradhishwa rakaa mbili mbili. Mtume akaiswali hivyo Makka mpaka alipofika Madina akaendela kuswali hivyo Madina kwa muda alioutaka Mwenyezi Mungu, ndipo zilipozidishwa katika Swala isiyu ya safari na ikaachwa Swala ya safari katika hali yake ile ile.”³¹

Toka kwa Jafar bin Umar amesema: Anas bin Malik alitupeleka Shamu kwa Abdul-Malik tukiwa watu arubaini toka watu wa Madina ili atufaradhishie, hivyo tulipofika Fajin-Naaqaa wakati wa kurejea alituswalisha adhuhuri rakaa mbili kisha akaingia hemani. Wakasimama watu na kuanza kuongeza katika rakaa zao rakaa mbili nyingine. (Anas) Akasema: “Mwenyezi Mungu aziharibu nyuso zenu, naapa kwa Mwenyezi Mungu! Hazikupatia Sunna wala hazikukubali ruhusa, shuhudia, hakika nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Hakika kuna watu watazama ndani ya dini kisha watachomoka kama uchomokavyo mshale toka kwenye upinde.”³²

Toka kwa Thamamat bin Sharahili amesema: Nilitoka kwenda kwa Ibnu Umar nikamwambia: Huwa vipi Swala ya msafiri? Akasema: “Rakaa mbili mbili isipokuwa Swala ya magharibi ndio huwa tatu.” Mpaka mwisho wa Hadith.³³

Toka kwa Abu Huraira amesema: “Enyi watu hakika Mwenyezi Mungu aliwafaradhishieni Swala kwa ulimi wa nabii wenu pasipo safarini rakaa nne.”³⁴

Toka kwa Ibnu Harbi amesema: “Nilimuuliza Ibnu Umar, ewe Aba Abdurahmani inakuwaje Swala ya safari?” Akasema: “Kama mnafu-

31. Rejea iliyotangulia, uk:156

32. Al-Imamu Ahmad: *Al-Musnadi*:3/159. *Majmuauz-Zawaid*:2/155

33. Al-imamu Ahmad: *Al-Musnadi*:2:154

34. Rejea iliyotangulia:2/400

Kupunguza Swala Safarini

ata Sunna ya Mtume wenu nitawaambia na kama hamfuati Sunna ya nabii wenu siwaambii. Tukasema: Kitu bora kinachofatwa ni Sunna ya nabii wetu. Akasema: “Mtume alikuwa atokapo nje ya Madina hazidishi rakaa mbili mpaka anaporejea humo.”³⁵

Toka kwa Saidi bin Al-Musayyibu, toka kwa Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Mbora wenu ni atakayepunguza safarini na asifunge.”³⁶

Haya ndio maelezo tuliyoyafikia toka kwa Mtukufu Mtume, maswahaba zake na waliokuja baada ya maswahaba kwa wema. Maelezo haya yamefuatwa na baadhi ya maswahaba na wengine kama vile: Umar bin Al-Khattab na mwanae, Ibnu Abbas, Jabir, Jubeiri bin Mutiim, Hasan, Al-Qadhiy Ismaili, Hamadi bin Abi Sulaimani, Umar bin Abdul-Aziz, Qatada na watu wa Kufa.³⁷

Naongezea kuwa Maimamu wa ahlul-Baiti wote na wanachuoni wa kishia kuanzia zama za Imamu Ali (a.s.) mpaka leo wote wamekubaliana na hilo.

Hivi baada ya Hadith hizi, je unaona kuna nafasi ya kusema kuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari na sio lazima!? Laiti ingekuwa inasihi kutimiza safarini basi Mtume angekuwa anabainisha hilo kwa kauli au kwa vitendo, angalau angefanya hivyo mara moja tu katika umri wake ili abainishe ruhusa ya kutimiza kama alivyofanya katika mambo mengine.

Muslim amepokea ndani ya *Sahih* yake toka kwa Buraida amesema: “Mtume alikuwa akitawadha kila wakati wa Swala, na ilipofika siku ya ukombozi wa Makka aliswali Swala zote kwa udhuu mmoja, Umar

35. *Musnad Ahmad*:2/124. *Al-Mughuniyu*:2/111

36. *Al-Mughuniyu*:2/111

37. Al-Qur'tubiy: *Al-Jamiu liah-kamil-Qur'an*:5/351

Kupunguza Swala Safarini

akamwambia: “Hakika wewe umefanya jambo ambalo hujawahi kuli-fanya.” Akasema: “Nimelifanya makusudi. (yaani kwa ajili ya kubainisha ruhusa ya hiyari).³⁸

Na laiti kama ruhusa ya kutimiza ingekuwepo basi isingefichika kwa maswahaba wakubwa na wala wasingewakosoa wenye kutimiza kukosoa kukali kwa namna hii. Hapo ndipo unafahamu thamani ya kigezo cha wenye kutimiza wasemapo kuwa kutimiza na kupunguza ni masuala ya kijiithadi (ya kielimu) ambayo wanachuoni wametofautiana.³⁹

KUPUNGUZA SWALA MINA

Kuna riwaya nyingi kuwa Mtume na makhalifa baada yake hata Uthman katika miaka yake ya mwanzo wote walikuwa wakipunguza wawapo Mina. Hivyo Uthman alipotimiza baada ya miaka minane lawama zilimshukia. Abdallah bin Mas’udi aliposikia kuwa Khalifa alitimiza Swala alipokuwa Mina alisema: “*Innaa lillahi wainna ilayhi raajiu’un!* (Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea!).

Neno hilo huwa halisemwi isipokuwa msiba unapouma, hii inaonyesha kuwa Abdallah bin Mas’udi alipokea kitendo cha Uthman kama msiba mkubwa ulioikumba dini. Na atakayefuatilia vizuri riwaya zitakazofuata ataamini kuwa walichokipokea maswahaba ni kuwa kupunguza ni lazima na kutimiza si ruhusa kisheria. Na laiti kama ingekuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari au ni Sunna tu basi maswahaba na waliokuja baada ya maswahaba wasingelalamikia kitendo cha Uthman.

38. *Sahih Muslim*:1/122. *Naylul-Awtari*:1/258

39. Muhibud-Dini At-Tabariy: *Al-Riyadhul-Nadhirati*:2/251

Kupunguza Swala Safarini

Muslim amepokea ndani ya *Sahih* yake toka kwa Salim bin Abdallah toka kwa baba yake kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali Swala ya msafiri rakaa mbili huko Mina na sehemu nyingine. Pia Abu Bakr na Umar waliswali rakaa mbili na Uthman mwanzoni mwa utawala wake, kisha baadaye akatimiza rakaa nne. ⁴⁰

Muslim amepokea toka kwa Ibnu Umar alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali rakaa mbili huko Mina, na Abu Bakr baada yake na Umar baada ya Abu Bakr na Uthman mwanzoni mwa utawala wake. Hakika Uthman baadaye aliswali rakaa nne.

Hivyo Ibnu Umar alipokuwa akiswali na imamu huswali rakaa nne na anaposwali peke yake huswali rakaa mbili.⁴¹ Na utaona huko mbele kuwa alikuwa akirudia Swala nyumbani kwake.

Muslim amepokea toka kwa Hafsa bin Aswimu toka kwa Ibnu Umar amesema: “Mtume aliswali Mina Swala ya msafiri na Abu Bakr na Umar na Uthman miaka minane, au miaka sita. Hafsa amesema: Ibnu Umar alikuwa akiswali rakaa mbili huko Mina kisha anaenda kulala. Nikamwambia Ewe ami yangu, ungeswali rakaa mbili nyingine baada ya hizo. Akasema: “Nikifanya hivyo nitakuwa nimetimiza Swala.” ⁴²

Muslim amepokea toka kwa Harith bin Wahabi Al-Khazaiy amesema: “Niliswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu huko Mina huku watu wakiwa wengi sana akaswali rakaa mbili huko Mina.”⁴³

40. *Sahihi Muslim*:1/122. *Naylul-awtari*:1/258

41. Muhibud-Din Al-Tabariy: *Al-Riyadhul-nadhirati*:2/251

42. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/209. kitabu cha Swala ya wasafiri mlango wa kupunguza Swala Mina

43. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/209. kitabu cha Swala ya wasafiri mlango wa kupunguza Swala Mina

Kupunguza Swala Safarini

Muslim ametoa toka kwa Abdurahmani bin Yazidi amesema: “Uthman alituswalisha rakaa nne huko Mina. Ibnu Mas’udi akaambiwa kuhusu hilo akasema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea. Kisha akasema: Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu huko Mina rakaa mbili na nikaswali na Abu Bakr Mina rakaa mbili, nikaswali na Umar bin Al-Khattab huko Mina rakaa mbili. Natamani zingepata hadhi rakaa mbili zenye kukubalika kuliko rakaa nne.”⁴⁴

An-Nawawi baada ya kauli “Natamani zingepata hadhi rakaa mbili zenye kukubalika kuliko rakaa nne,” amesema: “Hakika maana yake ni kuwa natamani Uthman angeswali rakaa mbili badala ya rakaa nne kama alivyokuwa akifanya Mtume, Abu Bakr, Umar na Uthman mwanzoni mwa utawala wake.

Kwa kuwa riwaya inaweka wazi kuwa alichokipokea Abdallah bin Mas’udi toka katika kitendo cha Mtume ni kuwa kupunguza ni lazima ndio maana akasema: *‘Inaa lillahi waina ilayhi raajiuun’* (Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea). Kisha akasema: “Natamani zingepata hadhi rakaa mbili zenye kukubalika kuliko rakaa nne.”

An-Nawawi na wengine wamejaribu kubeua riwaya na kupunguza mkanyago akasema: Makusudio yake ni kuchukizwa na kitendo cha kukhalifu kile alichokichagua Mtume na maswahaba zake wawili. Hivyo kwa maana hii ni kuwa Ibnu Mas’udi anaafiki ruhusa ya kutimiza, na kwa ajili hiyo ndio maana alikuwa akiswali kamili nyuma ya Uthman na laiti kama kupunguza kungekuwa ni wajibu kwake basi asingekubali kuacha kupunguza nyuma ya yoyote.

44. *Sahih Bukhari:2/53*, mlango wa kupunguza. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/209. kitabu cha Swala ya wasafiri mlango wa kupunguza Swala Mina.

Kupunguza Swala Safarini

Ni wazi kuwa aliyoyasema An-Nawawi ni kukimbia haki wazi wazi, kwani haitokuwa na maana yoyote (Ibnu Mas'udi) kuomba kurejea na wala kutamani iwapo kama kitendo cha khalifa Uthman ni sahihi kisheria, kimeruhusiwa na sheria na kikafundishwa na Mtume isipokuwa kwa sababu ya ruhusa ya hiyari ikawa Mtume amechagua kilicho bora zaidi huku akiwa hajakataza hiki kingine.

Kisha kile kilichonasibishwa na Abdallah kuwa alitimiza Swala safarini pindi aliposwali na Uthman hakika ilikuwa ni kulinda siasa ya kutokukhalifu kutokana na Uthman kuona kuwa kung'ang'ania kupunguza ni kukhalifu rai yake. Aamashi amesema: “Amenisimulia Muawiya bin Qarat toka kwa mashekhe wake kuwa Abdallah aliswali rakaa nne, akaambiwa: Umemkosoa Uthman kisha umeswali rakaa nne? Akasema: “Kukhalifu ni kuleta shari.”⁴⁵

Pia ndio hali ya Abdallah bin Umar. Ibnu Hazimu amesema: “Tumepokea kwa njia ya Abdur-Razaq toka kwa Abdallah bin Umar toka kwa Nafiu toka kwa Ibnu Umar kuwa alikuwa anaposwali na imamu rakaa nne huko Mina huenda nyumbani kwake na kuswali rakaa mbili kwa kurudia Swala.”⁴⁶

Hawa walikuwa wanaona kulinda masuala ya kisiasa ili kuepuka shari ni bora kwao kuliko kuhifadhi hukumu za dini kama zilivyoteremka toka kwa Mwenyezi Mungu na kusimama kidete ili zisibadilishwe na kugeuzwa.

Isipokuwa baadhi ya maswahaba walikuwa kinyume na hilo, kwani huyu hapa Ali anakataa kuswali rakaa nne huko Mina japokuwa Uthman na Bani Umayya walimsisitiza afanye hivyo. Akaambiwa: Wasalishe watu. Akasema: “Mkitaka basi nitawasalisheni Swala ya

45. *Sunnani Abu Malik*:1/308. *Kitabul-Umi* cha Shafiy:1/159

46. *Al-Mahaliy*:4/270.

Kupunguza Swala Safarini

Mtume wa Mwenyezi Mungu.” (Yaani raka mbili) Wakasema: “Hapana isipokuwa Swala ya kiongozi wa waumini raka nne.” (Yaani Uthman) Akakataa Swala ya Uthman. ⁴⁷

Hakika Bani Umayya wamefanya uzushi huu wa Uthman kuwa ni Sunna yenye kuendelea milele mkabala na Sunna ya Mtume hata kama hawana udhuru wa kisheria unaowaruhusu kutimiza.

Imamu Ahmad bin Hambali ametoa ndani ya *Musnadi* yake toka kwa Abdallah bin Zubeir kuwa alisema: “Alipokuja Muawiya kuhiji tulienda naye Makka. Akasema: Akatuswalisha adhuhuri raka mbili kisha akaenda Darun- Naduwa. Akasema: Wakasimama Marwan bin Al-Hakam na Umar bin Uthman wakamwambia: “Hakuna mtu aliye-muaibisha mtoto wa ami yako kwa jambo baya kama ulilomuaibisha kwalo.”

Akasema: “Ni jambo gani hilo?” Wakamwambia: “Hivi hujui kuwa alitimiza Swala Makka.” Akawaambia: “Ole wenu, Je Swala ilikuwa ni kinyume na nilivyofanya? Hakika niliziswali raka mbili nikiwa pamoja na Mtume, na pamoja na Abu Bakr na Umar.” Wakasema: “Hakika mtoto wa ami yako alikuwa ameshazitimiza hivyo kumukhalifu kwako ni kumuaibisha.” Akasema: “Muawiya akatoka kutuswalisha alasiri akatuswalisha raka nne.”⁴⁸

Mpaka hapa zimetimia Hadith na riwaya zinazoonyesha kuwa kupunguza safarini ni lazima na kutimiza ni uzushi uliozushwa baada ya kufariki Mtume kwa sababu ya ijthadi au kwa sababu ya kufuata maslahi ya kutoleta utengano. Hivyo mwanachuoni wa fiq’hi hana njia isipokuwa ni kufuata na kunyenyekea, kwanza mbele ya kitendo cha kudumu cha Mtume, pili mbele ya riwaya hizi .

47. *Al-Mahaliy*: 4/270

48. *Musnad* Ahmad bin Hambali: 4/94

Kupunguza Swala Safarini

Baada ya hapo imebakia tutoe dalili za wanaosema kuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari au Sunna iliyohimizwa na wala si lazima, nazo ni dalili mbovu sana ambazo haisihi kwa mwanachuoni wa fiq'hi kuzitegemea ikiwa kweli anajua kutoa sheria toka ndani ya vyanzo vyake.

DALILI ZA WANAODAI KUWA KUPUNGUZA NI RUHUSA YA HIYARI

Hawa wametoa hoja mbalimbali baada ya Kitabu, nasi tutazitaja moja baada ya nyingine.

Ama Kitabu kitukufu, ni kuwa nimeshazungumzia hilo kuwa hakika Aya haijulishi moja kati ya kauli mbili yaani ruhusa ya hiyari na lazima. Bali Aya imekuja kuondoa dhana ya uharamu, kwani kupunguza Swala kulileta dhana ya kuwa ni kuleta upungufu ndani ya Swala. Hivyo Mwenyezi Mungu akabainisha kuwa si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala. Ni wapi Aya hii imejulisha kuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari.

Hakika dalili zao muhimu ni riwaya zilizopokewa, nazo ni kama hizi zifuatavyo:

Muslim amepokea toka kwa Yaaliy bin Umayya amesema: “Nilimwambia Umar bin Al-Khattab: “Na mnaposafiri katika ardhi basi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala, iwapo mkiogopa ya kwamba wale waliokufuru watakupeni taabu. Akasema: “Lilinishangaza lile lililokushangaza hivyo nikamuuliza Mtume, akasema: “Ni sadaka aliyowaneemesha Mwenyezi Mungu pokeeni sadaka yake.”⁴⁹

49. *Sharhu Muslim* ya An-Nawawi: 5/203, namba 4.

Kupunguza Swala Safarini

Hoja: Hakika mwenye kupewa sadaka si lazima kupokea sadaka.

As-Shaukaniy amejibu hoja hiyo kwa kusema: Hakika kitendo cha kuamrisha kupokea ni dalili ya kuwa ni lazima kupokea na ndilo linalotakiwa. ⁵⁰

Ilimpasa As-Shaukaniy aongeze kumjibu kwa njia nyingine aseme: Kulinganisha sadaka na zawadi ya Mwenyezi Mungu na sadaka na zawadi za watu ni kulinganisha vitu visivyofanana. Kwa sababu mwenye kupewa sadaka au kupewa zawadi si lazima kupokea iwapo mtoaji ni mwanadamu mwenzake.

Ama kama mtoaji sadaka ni Mwenyezi Mungu ni lazima kuipokea, kwa sababu sadaka ya Mwenyezi Mungu ni jambo la neema, na kuneemesha kwa Mwenyezi Mungu hakuwi bila sababu na lengo. Bali kunatokana na hekima ya juu ya Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu anajua masilahi ya asili ya mwanadamu yanahitaji neema hiyo anayowaneemesha waja wake, hivyo kuipokea inakuwa ni lazima kwao.

Na inadhihiri katika Hadith za Ahlul-Baiti kuwa kukataa sadaka ya Mwenyezi Mungu ni haramu, kwani Imam Jafar Sadiq (a.s.) amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hakika Mwenyezi Mungu alimpa sadaka mgonjwa na msafiri wa umma huu kwa kumpa kupunguza na kufungua, hivi inamfurahisha mmoja wenu kukataliwa sadaka atakapotoa.?” ⁵¹

Ni kama kwamba katika kukataa sadaka kuna aina fulani ya dharau kwa mtoaji wa sadaka, na katika maudhui yetu hii ni kuifanyia ujeuri sheria ya Mwenyezi Mungu.

50. *Naylul-Awtari*:3/201

51. *Wasailus-Shia*:1/175

Kupunguza Swala Safarini

Ad-Darqutniy na Al-Bayhaqiy wametoa na tamko ni la wa kwanza toka kwa Abdurahmani bin Aswad toka kwa Aisha amesema: “Nilitoka na Mtume kwenda Umra ndani ya Ramadhani akala, mimi nikafunga, akapunguza mimi nikatimiza. Nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimekufidia baba na mama, umefungua na mimi nimefunga, umepunguza na mimi nimetimiza.” Akasema: “Umefanya vizuri ewe Aisha.”⁵²

As-Shawkany amesema: “Riwaya hii pia ameitoa An-Nasaiy na Al-Bayhaqiy kwa nyongeza kidogo: Hakika Aisha alikwenda Umra na Mtume toka Madina hadi Makka, walipofika Makka Aisha alisema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nimekufidia baba na mama, nimetimiza na umepunguza.”

Hoja ya riwaya inategemea, kwanza usahihi wa mtiririko wa wapokezi na pili uwezekano wa kuchukua madhumuni yake. Ama upande wa mtiririko wa wapokezi ni kuwa yumo Al-Alau bin Zuhair toka kwa Abdurahmani bin Aswad bin Yazid An-Nakhaiy toka kwa Aisha.

Ibnu Habbani amesema: “Alikuwa akipokea toka kwa wapokezi waaminifu Hadith zisizoafikiana na wapokezi waaminifu, hivyo yeye si hoja katika zile zisizoafikiana na wapokezi waaminifu.”

Ad-Darqutniy amesema: “Mtiririko huu wa wapokezi ni safi, na Abdur-rahman alimdiriki Aisha na akaingia kwake yeye na baba yake akiwa bado mtoto anayekaribia balehe na alisikia toka kwake.”⁵³

Abu Hatimu amesema: “Aliingia kwake akiwa mtoto mdogo wala hakisikia toka kwake.” Vipi itawezekana kuchukua kauli ya mpokezi

52. *Sunnanid-Darqutny*:2/188. *Al-Sunnanil-al-Kubra*:3/142

53. *Sunnani Darqutny*:2/188, namba 40.

Kupunguza Swala Safarini

ambaye haujathibiti usikivu wake toka kwa Aisha? Na hata tukijaalia kuwa amesikia lakini kasikia akiwa mtoto mdogo au mtoto anayekaribia balehe.

Kwa ajili hiyo ndio maana Ad-Darqutniy ndani ya kitabu *Al-Ilali* amedhania kuwa ni Hadith ya kuvushwa. (Mursalu. Yaani isiyoyana na mtiririko mzima wa wapokezi). Maelezo hayo ni kama alivyoyanukuu As-Shawkany toka kwake ndani ya kitabu *Nailul-awtari*.⁵⁴

Na kinachozidisha tope za udongo maji ni kuwa Ad-Darqutny mara kapokea toka kwa Abdur-rahman toka kwa baba yake toka kwa Aisha, na mara nyingine kapokea toka kwa Abdur-rahman toka kwa Aisha.⁵⁵

Al-Bayhaqi kanukuu toka kwa Abu Bakr An-Nisaburiy kuwa atakayesema kuwa kapokea Hadith hii toka kwa baba yake atakuwa kakosea.⁵⁶

Dosari zote hizi ni kuhusu mtiririko wa wapokezi (*Sanadi*).

Ama madhumuni ya Hadith, kwanza tunajibu kuwa: Katika Hadith ya Aisha imepokewa kuwa: Nilitoka na Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda Umra ndani ya Ramadhani.....mpaka mwisho.

Suala hili moja kwa moja linapingana na historia ya mwenendo wa Mtume. Ndani ya kitabu *As-Siratul-Halabiyya* imeandikwa: “Hakuna shaka kuwa Umra ya Mtume haikuwa zaidi ya mara nne, yaani mara zote ndani ya mfunguo pili kwa ajili ya kuwakhaliifu mushrikina kwani hakika wao walikuwa wakichukizwa kufanya Umra katika miezi ya Hijja wakisema kuwa ni kati ya makosa makubwa.....

54. *Naylul-awtari*:3/202

55. *Sunnanid-Darqutny*:2/188 namba 39 na 40

56. *As-Sunnanil-Kubra*:3/142

Kupunguza Swala Safarini

Na Umra ya kwanza kati ya hizo nne ni Umra ya Al-Hudaibiyya ambayo ilikuwa mfungo pili ambayo mushrikina walimzuia Mtume.

Na ya pili ni Umra yake ya mwaka uliofuatia nayo ni Umra ya kulipa nayo ilikuwa mfunguo pili.

Na ya tatu ni Umra yake alipogawa mali waliyoipata katika vita vya Hunaini naye alitokea Al-Jaarana na ilikuwa mfunguo pili.

Na ya nne ni Umra iliyoambatana na Hijja yake ya mwisho hakika ali-
vaa ihramu siku tano kabla ya kumalizika mfunguo pili.

Na Aisha amesema: “Mtume alikwenda Umra mara tatu isipokuwa ile aliyoikutanisha na Hijja ya kuaga.”⁵⁷

Kutokana na maelezo haya itakuwaje tuchukue madhumuni ya Hadith hii ilihali hakuna Umra yoyote aliyoifanya Mtume akiwa na mkewe ndani ya mwezi wa Ramadhani.

Amesema ndani ya *Al-Badrul-muniru*: “Hakika matamko ya Hadith hii hayakubaliki, nayo ni kuwa Aisha alitoka pamoja naye kwenda Umra mwezi wa Ramadhani, Na mashuhuri ni kuwa hakwenda Umra isipokuwa mara nne na kati ya zote nne hakuna ya Ramadhani bali zote zilikuwa mfunguo pili isipokuwa ile aliyoikutanisha na hija yake. Hivyo ihramu yake ilikuwa mfunguo pili na akafanya Umra ndani ya mfunguo tatu. Na hili ndilo maarufu ndani ya *Sahih* mbili (Bukhari na Muslim) na ndani ya vitabu vingine.”⁵⁸

Pili: Ilikuwaje Aisha atimize na afunge huku Mtume na maswahaba zake wamepunguza na kufungua ilihali kitendo chake hakikuwa ni

57. *Siratul-Halabiyya*: 3/240- 241

58. *Naylul-awtari*:3/202 Amenukuu toka *Al-Badrul-Muniri*

Kupunguza Swala Safarini

cha siku moja, bali kwa mujibu wa riwaya ilikuwa ni kitendo cha siku nyingi toka Madina mpaka Makka ilihali misafara ilikuwa ikitumia mwendo wa siku kumi kati ya miji hiyo miwili?

Je inaingia akilini kuwa mama wa waumini alimukhalifu Mtume na maswahaba ilihali Mtume na wengine wakiwa mbele yake akiwaona na kuwasikia?

Kwa ajili hiyo ndio maana Ibnu Taymiyya amesema: “Hadithi hii ni uongo amezushiwa Aisha, wala Aisha alikuwa haswali kinyume na Mtume wala kinyume na maswahaba ilihali anawashuhudia wakipunguza kisha atimize peke yake bila sababu ya kuwajibisha hilo.”

Itakuwaje afanye hivyo ilihali amesema: “Swala ilifaradhihwa raka mbili mbili ikazidishwa Swala isiyo ya safari na ikasitishwa Swala ya safari?! Itakuwaje idhaniwe kuwa yeye anaweka nyongeza kwenye faradhi ya Mwenyezi Mungu na anamukhalifu Mtume wa Mwenyezi Mungu na maswahaba zake!?”⁵⁹

3. Darqutny ametoa toka kwa Muhammad bin Mansuri bin Abil-Jahami kuwa alitusimulia Nasri bin Ali, alitusimulia Abdallah bin Malik toka kwa Al-Mughira bin Ziyada Al-Muswiliy toka kwa Atau toka kwa Aisha kuwa: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akitimiza safarini na akipunguza. Kisha akasema: Al-Mughira bin Ziyada Al-Muswiliy si mwaminifu.⁶⁰

4. Abu Daud At-Twayalisiy amesema: Ametusimulia Yunus, amesema: Ametusimulia Abu Daud, amesema: Ametusimulia Twalha amesema: “Nilimsikia Atau akisimulia toka kwa Aisha kuwa alisema: Hayo yote aliyafanya Mtume safarini, alifunga na alifungua.”⁶¹

59. Ibnul-Qaymul-Jawziyya: *Zadul-miadi*:1/161. *Naylul-awtari*:3/20

60. *Sunnanid-Darqutny*:2/189

61. *Musnad Twayalisiy*: 6/609 chapa ya Makka.

Kupunguza Swala Safarini

Ad-Darqutny ameinukuu kwa mtiririko huu japo kwa tofauti kidogo katika matamko. Kisha mwisho wake akasema: “Twalha ni dhaifu.” (si mwaminifu) ⁶²

Riwaya mbili hizi zinajibiwa kuwa: Mtiririko wa wapokezi wenyewe tu si hoja baada ya kujua kuwa Al-Mughira na Twalha si waaminifu.

Na hata tukijaalia kuwa ni hoja lakini haziwezi kuvunja kauli na vitendo vilivyopokewa toka kwa Mtume tu. Kama vile zisivyoweza kuvunja Hadith zilizopokewa toka kwa maswahaba kuwa Mtume umri wake wote alikuwa akipunguza safarini. Kama zilivyotangulia riwaya kuhusu hilo.

Ama dalili ni kuwa riwaya hizo hazina dalili yoyote kuhusu kutimiza kwa sababu hata kama Aisha amepokea kitendo cha Mtume kuwa alikuwa anatimiza, lakini inawezekana kutimiza kwake ni kwa sababu alikuwa hajatimiza sharti zote za kupunguza safarini.

Na imeshathibiti kuhusu vitendo kuwa kitendo chake hakiwi hoja mpaka ijulikane lengo na sababu. Na kitendo chake katika riwaya hizo mbili kimejifunga sana, hivyo inawezekana kutimiza kwake ilikuwa ni kwa ajili ya ruhusa ya hiyari safarini au kwa ajili ya kuto-timia sharti za kupunguza.

Kisha Ibnu Hazmi ndani ya *Al-Mahaliy* ana maneno kamilifu kuhusu riwaya hizi kwani amesema: “Ama ambayo imekuja kwa njia ya Abdur-rahman bin Al-Aswad kaipokea Al-Alau bin Zuhair Al-Azdiy peke yake hakuna mwingine aliyeipokea ilihali yeye mwenyewe hajulikani.

62. *Sunnanid-Darqutny*: 2/189.

Kupunguza Swala Safarini

Ama Hadith ya Atau ameipokea Al-Mughira peke yake hakuna mwingine alieipokea. Na Ahmadi bin Hanbali amemzungumzia kwa kusema: Yeye ni dhaifu kila Hadith zilizopitia kwake hazikubaliki.

4. Aliyoipokea An-Nawawi katika ufafanuzi wake wa *Sahih Muslim* amesema: “Hakika maswahaba walikuwa wakisafiri na Mtume wa Mwenyezi Mungu, hivyo baadhi yao wanapunguza na wengine wanatimiza, baadhi yao wanafunga wengine wanafungua bila kukosoana.”⁶³

Ibnu Quddama amenukuu toka kwa Anas kuwa alisema: “Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu tulikuwa tukisafiri huku baadhi yetu wanatimiza na wengine wanapunguza, baadhi yetu wanafunga na wengine wanafungua wala hakuna anayemkosoa mwenzake.”

Kisha akasema: “Kwa mujibu wa Hadith ya Anas ni kuwa suala hilo ni ijimai ya maswahaba kwa kuwa wapo waliyokuwa wakitimiza Swala na wala waliobaki hawajakataza.”⁶⁴

As-Shawkany amesema: “Hoja ya tatu juu ya kuruhusu kutimiza ni riwaya iliyomo ndani ya *Sahih Muslim* na vitabu vingine kuwa maswahaba walikuwa wakisafiri na Mtume wa Mwenyezi Mungu huku miongoni mwao wakiwa wamo waliopunguza na wengine wametimiza, wengine wamefunga na wengine wamefungua wala hawakosoani.”⁶⁵

Anajibiwa kuwa: Muslim ametoa riwaya saba ndani ya mlango wa Swaumu na kufungua ndani ya mwezi wa Ramadhani kwa msafiri toka kwa Abu Saidi Al-Khidriy, Jabir bin Abdillahi Al-Answariy na

63. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi: 5/201. Kitabu cha Swala ya msafiri.

64. *Al-Mughuni*:2/109.

65. *Naylul-awtari*:3/2010202. Na An-Nawawi ameitaja ndani ya *Shar'hu Sahih Muslim*.

Kupunguza Swala Safarini

Anas bin Malik, ndani ya riwaya hizo hakuna inayozungumzia kupunguza na kutimiza, bali zinazunguka kwenye saumu na kufungua, hivyo haijadhihiri kwangu chanzo cha sentensi iliyonasibishwa na Anas (baadhi yetu wanatimiza na wengine wanapunguza).⁶⁶

Tunataja mfano tu wa baadhi ya hizi riwaya. Anas (R.A) aliulizwa kuhusu funga ya Ramadhani safarini, akasema: “Tulisafiri na Mtume ndani ya Ramadhani mwenye Saumu hakumkosoa asiye na Saumu wala asiye na Saumu hakumkosoa mwenye Saumu.”

As-Shawkany amesema: Wala ndani ya *Sahih Muslim* hatujakuta kauli: “Miongoni mwao wakiwa wamo waliopunguza na wengine wametimiza. Wala hamna isipokuwa Hadith za saumu na kufungua.”⁶⁷

Na tujaalie kuwa yaliyonasibishwa na Muslim ni sahihi, lakini ni wapi imethibiti kuwa Mtume alikiona kitendo chao na hivyo akakiunga mkono mpaka kiwe ni uthibitisho ulio hoja kwetu? Wala kitendo cha maswahaba tu si hoja, ni mpaka ithibiti kuwa kimetokana na kauli ya Mtume na kitendo cha Mtume.

As-Shawkany amesema: “Ijmai ya maswahaba kipindi cha zama zao si hoja kwani ni mashuhuri kutokukubaliana kwao baada ya kifo chake (Mtume).”⁶⁸

66. Angalia *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:7/237, mlango wa ruhusa ya saumu na kufungua katika mwezi wa Ramadhani kwa msafiri. Hadithi ya 93 mpaka 99. Angalia *Sahih Muslim*: 3/143, kitabu cha Swaumu, mlango wa ruhusa ya saumu na kufungua ndani ya mwezi wa Ramadhani kwa msafiri.

67. *Naylul-awtari*:3/202

68. *Naylul-awtari*:3/202

Kupunguza Swala Safarini

Mpaka hapa zimetimia hoja zinazoweza kuwa dalili ya kutimiza safarini, na tayari umeshajua kuwa zote ni mangati wala si maji, hivyo haziwezi kuwa hoja sahihi mbele ya riwaya na Hadith nyingi ambazo zimepokewa kwa njia mbalimbali zinazoishia kwa maswahaba.

Ibnu Hazimu amesema: “Na tumezipokea pia kwa njia ya Hudhaifa, Jabir, Zaidi bin Thabit, Abu Huraira na Ibnu Umar wote wametoa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mtiririko uliyoko kwenye kilele cha usahihi. ⁶⁹

Hapa limebakia jambo lingine nalo ni kushikilia kitendo cha swahaba wa kiume na swahaba wa kike. Na ufatao ni ufafanuzi wake.

KUTOA HOJA KWA KUTUMIA KITENDO CHA UTHMAN NA AISHA

Huenda mtu akatoa hoja juu ya kutimiza kwa kutumia kitendo cha Uthman ambaye alitimiza Makka na Mina japokuwa alikuwa msafiri na ameshahama Makka huku akiwa mkazi wa Madina.

HOJA HII INAJIBIWA KUWA: Hakika kitendo cha swahaba si hoja ikiwa hakijatokana na Hadith sahihi toka kwa Mtume, kwani hakika hoja ni kitendo cha mtakasifu si mwingine. Zaidi ya hapo ni kuwa Uthman alilaumiwa juu ya hilo, na maswahaba wengi wakampinga mpaka Abdallah bin Mas’udi akaomba kurejeshwa.

Na linalojulisha kuwa Uthman alitimiza kwa matakwa yake binafsi bila ya dalili sahihi ni ile riwaya aliyoitoa Muslim toka kwa Az-Zahriy toka kwa Urwa toka kwa Aisha.

⁶⁹.Al-Mahaliy:4/271

Kupunguza Swala Safarini

Az-Zahriy amesema: “Nikamwambia Urwa kwa nini Aisha anatimiza safarini. Akasema: Alibeua kama alivyobeua Uthman.”⁷⁰

Ibnu Hazimu ameinukuu ndani ya *Al-Mahaliy* kuwa amesema Az-Zahriy, nikamwambia Urwa: “Kwa nini Aisha alitimiza safarini ilihali ameshajua kuwa Mwenyezi Mungu alifaradhisha rakaa mbili mbili?” Akasema: ‘Alibeua katika hilo kama alivyobeua Uthman kwa kutimiza Swala Mina.’⁷¹

Hivyo laiti Uthman angekuwa na dalili ya kuruhusu kutimiza angeitoa na wala asingekimbilia kubeua maana. Na hii ni dalili kuwa kupunguza safarini ndio kunakotakiwa lakini yeye alitimiza kwa kigezo maalum anachokijua mwenyewe.

Wapo wengi waliosimama kutaka kujaribu kutetea kitendo cha khalifa na mama wa waumini kwa kuwawekea udhuru.

An-Nawawi amesema: “Wanachuoni wametofautiana kuhusu vigezo vya kubeua kwao: Sahihi ni kile walichokichukua watafiti wa dini, nacho ni: Waliona kuwa kupunguza ni ruhusa na kutimiza ni ruhusa hivyo wakachukua moja kati ya ruhusa mbili nayo ni kutimiza.

Wanajibiwa kuwa: Huko si kubeua, kwani laiti kama kungekuwa na dalili za kuruhusu kutimiza basi ilipasa wazitumie kama hoja bila kubeua.

Na kwa ajili hiyo ndio maana walibeua kitendo cha khalifa na mama wa waumini kwa vigezo vingine, ninakusudia:

70. *Al-Mahaliy*: 4/271

71. *Sharhu Sahih Muslim* ya An-Nawawi:5/202 kitabu cha Swala ya msafiri

Kupunguza Swala Safarini

2. Hakika Uthman ni imamu wa waumini na Aisha ni mama yao hivyo ni kama raka mbili (za ziada) ndio ziko kwenye hadhi yao.

Anajibiwa kuwa: Mbeuaji amesahau kuwa Mtume ndiye aliyefaa zaidi kuliko wao wawili lakini kwa nini alipunguza daima?

3. Uthman alioa mke toka Makka.

Anajibiwa kuwa: Hali hiyo ni kama ya jibu lililopita kwani hakika Mtume alisafiri na wakeze miongoni mwao akiwemo wa Makka lakini alipunguza.

4. Alifanya hivyo kwa sababu ya mabedui ambao walikuwa naye ili wasije wakadhani kuwa Swala imefaradhishwa raka mbili daima safarini na pasipo safarini.

Anajibiwa kuwa: Maana na hali hiyo ilikuwepo tangu enzi za Mtume bali hali ya Swala enzi za Uthman ilikuwa mashuhuri kuliko ilivyoelezwa.

Na vigezo vingine zaidi ya hivyo vibovu ambavyo hawezi msomi wa fiq'hi akavitegemea, vigezo ambavyo kavinukuu imamu An-Nawawi ndani ya kitabu chake na akavibatilisha vyote isipokuwa kigezo cha kwanza. Tayari umeshaona kuwa nacho si sahihi. ⁷²

Kwa ajili hiyo inathibiti kuwa kitendo cha swahaba Aisha hakiwi hoja japokuwa amepokea kwamba Mwenyezi Mungu alifaradhisha Swala raka mbili mbili, ikasitishwa Swala ya safari na ikazidishwa Swala isiyo ya safari. ⁷³

⁷² *Al-Mahaliy*: 4/270

⁷³ *Sharhu Sahih Muslim*. Mlango wa Swala ya msafiri na kupunguza

Kupunguza Swala Safarini

Ibnu Jariri Tabariy ana maneno kuhusu kitendo cha Aisha ameyasema kwenye tafsiri ya kauli: [Mtakaposafiri aridhini] Kwa njia yake toka kwa Umar bin Abdallah bin Muhamnad bin Abdur-rahman bin Abu Bakr Sidiqi amesema: “Nilimsikia baba yangu akisema: Nilimsikia Aisha akisema: Safarini timizeni Swala zenu. Wakasema: Hakika Mtume anaswali safarini rakaa mbili. Akasema: Hakika Mtume alikuwa vitani na alikuwa na khofu, je ninyi mna khofu?”⁷⁴

As-Shawkany akaongeza kwa kusema: Imesemekana kuhusu kubeua kwa Aisha kuwa Hakika yeye alitimiza katika safari yake ya kwenda Basra kumpiga vita Ali (a.s.) na hakika kupunguza kwake huwa kwenye safari ya utiifu.

Mpaka aliposema: Ama kigezo bora cha mbeuo wa Aisha kati ya vigezo vilivyotajwa ni kile alichokitoa Al-Bayhaqiy kwa njia sahihi toka kwa njia ya Hisham bin Urwa toka kwa baba yake kuwa alikuwa anaswali rakaa nne safarini, nikamwambia: Ungeswali rakaa mbili. Akasema: ‘Ewe mtoto wa dada yangu hakika haziwi nzito kwangu.’⁷⁵

Nayo inaonyesha kuwa alibeua kuwa kupunguza ni ruhusa ya hiyari na kutimiza ni bora kwa yule asiyepatwa na uzito.⁷⁶

74. *Shar'hu Sahihi Muslim.*

75. *Tafsiri Tabariy:4/155*

76. *Naylul-awtari:3/212*

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA

NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na Nane
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

Kupunguza Swala Safarini

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillahi ni sehemu ya Qur'ani
45. Sauti ya uadilifu wa Binadamu
46. Kufungua Safarini.
47. Kusujudu juu ya udongo.
48. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Maulidi
51. Assalaatu Khayrumminan.
52. Uadilifu wa Maswahaba

BACK COVER

Kupunguza Swala Safarini:

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema: **"Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu." (5:3).**

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wamehitilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limesababisha kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya mwandishi amejaribu kuliweka suala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu.

Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata isababishe kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiislamu. Na mwongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

"Na shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu,

Kupunguza Swala Safarini

hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu." (3:103)

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

P.O. Box 19701

Dar es Salaam, Tanzania

Simu:+255 22 2110640

Simu/Fax: +255 22 2127555

Email: alitrah@raha.com

Website: www.alitrah.org

Online: www.alitrah.info